Hon. Jambo: Asante, Bw. Spika, kwa kunipa nasafi nami niweze kutoa changizo yangu. Kwa hakika, jamii ya Jaribuni inateseka. Kama Bunge hili linaweza kupeana mamlaka au kusaidia, sote tuunge mkono hii Ripoti ili tuweze kuokoa wale ndugu zetu walio kule Wadi ya Jaribuni. Ukitazama zile kampuni ambazo ziko kama Mwenyekiti alivyosema na kwa Ripoti ambayo imenakiliwa, umbali wa kampuni na mahali shule iko ni umbali wa chini ya mita Hamsini (50).

Itakuwa ni maandhari gani kwa yule mwanafunzi kuweza kusoma ikiwa huku kampuni inaendelea kuvunja mawe ama kelele zile zinzofanywa na kampuni? Yuko msomi aliyesema kwamba elimu ndio silaha muhimu ya kubadilisha ulimwengu. Sisi leo tuko katika Bunge hili tukufu na tuko hapa kwa sababu na kwa muda huu. Wale watoto wadogo wa Jaribuni ambao ndio viongozi wa kesho wanakosa haki yao ya elimu kwa sababu ya kampuni zinazotengeza fedha. Si jambo la busara, wala la kufungia macho. Lazima tutazame kwa jicho lengine kuona ya kwamba tunawapatia haki hata vizazi vya kesho kwa sababu hao ndio viongozi watakuja kushikilia baada ya sisi kukaa hapa.

Kazi ngumu inayofanywa na wazee kwa maboma yao kumtengezea kura za baadaye Mheshimiwa Shehe, unapata wamama wanaavya mimba, inatoka bila kutarajia kwa sababu ya kampuni. Ni swala la huzuni, sasa kama tuliletwa hapa ulimwenguni kwa sababu tujaze ulimwengu na kuna watu wanatengeza pesa huku mimba zinatoka...

(Hon. Ms.) Grace stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Mwambire): There is an intervention here.

Hon. (Ms.) Grace: Asante, mheshimiwa Spika. Ningelipenda mheshimiwa aliye kwenye Sakafu atueleeze hii kazi ngumu ambayo wazee wa Jaribuni wanafanya ni kazi ya kuchimba mawe ama ni kazi gani?

(Laughter)

Hon. Jambo: Asante. Nafikiri kwa kumuelimisha ni kwamba kazi ngumu ni ya kutengeza watoto, nilikuwa namaanisha hivyo...

(Hon. Shehe stood on a Point of Information)

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Shehe also wants to make an intervention ama hamtoki jasho? ...

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Shehe: Thank you, hon. Speaker. I have a very practical example that I would like to share with my hon. Members...

The Speaker (Hon. Mwambire): Then it is a Point of Information. Do you wish to be informed?

Hon. Jambo: No, no...

The Speaker (Hon. Mwambire): Sorry hon. Shehe, he is not willing to be informed. Just take your seat. *Endelea. mheshimiwa Jambo.*

(Laughter)

Hon. Jambo: Nafikiri angeniwacha nikamaliza. Nikiongezea ni kwamba tuna uhitaji wa kusaidia ile jamii ukiangalia kama Mto Nzovuni, chemichemi za maji zimekauka. Binadamu ni maji na maji ni uhai. Maji yamekauka kwa sababu ya kazi inayoendelea pale na kampuni zile. Kuna umuhimu ile mito ambayo inasaidia jamii kupata maji tuweze kusimamisha zile kazi. Ningeomba Bunge hili ya kwamba Ripoti hii ambayo imeweza kuletwa tuiunge mkono ili jamii ya Jaribuni iweze kusaidika kama wengine ndani ya Kaunti ya Kilifi. Asante.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Morris Hinzano, Member for Kakuyuni.

Hon. Hinzano: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia hii nafasi. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na afya tele. Kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri ambayo imefanya juu ya swala hili la machimbo kule Jaribuni. Ni aibu sana na ni huzuni kwa muda wa wiki mbili imepita mpaka sasa tulikuwa tukijadili jinsi Kaunti yetu imevamiwa na wakora ambao wanaibia Kaunti ya wale mashirika ya NARIGP (*National Agricultural and Rural Inclusive Growth Project*). Mambo mengi tulikuwa tunajadili hii wiki na wiki iliyopita ni kuhusu watu kuiba, hakuna mpango mwingine. Watu walikuwa wanaiba, kuficha stakabadhi. Saa hii wakora wako wanaoibia Kaunti na pia wauaji.

(Laughter)

Mheshimiwa Spika, hili swala si la kuchekesha na ni huzuni sana ikiwa sheria imewekwa na ikaambiwa hayo mashirika yafungwe kwa sababu ya kudhuru maisha ya wananchi lakini yanaendelea tu. Ni nani mwenye uwezo anayeweza kupingana na sheria na kuendeleza na kazi ya machimbo yaendeleo na kuna Serikali ya Kaunti ambayo tunaiamini na pia ikishindikana kuna Serikali ya Kitaifa. Watu wanaendelea kuumia na kufa. Hilo halionekani; linaloonekana hapa ni fedha ziingie ili kwamba mambo fulani yaendeleo. Yataendelea vipi na yatakuwa yanamfanyia nani hayo maendeleo ikiwa wananchi wanakufa?

Mheshimiwa Spika, mahali imefikia sasa hivi mbali na Waziri kupatiwa hiyo Ripoti na hakuna Ripoti inayofanyika ya maana, ni maoni tu japo Ripoti ni nzuri lakini tusimame kama Bunge twende hapo Jaribuni kwa hizi kampuni zote kama Wabunge wa Kaunti ya Kilifi na kuweza kuyafunga. Kama watatupeleka jela, ni badaye lakini tujulikane kwamba tunatetea watu wetu maanake kama hawawezi kufuata sheria kwa sababu ziko kwa makaratasi tuende wenyewe tukawambie tumesema hivi na haya mambo lazima yasimame la sivyo, wananchi wanaumia. Tutaongea, hapa kuna wakubwa wataenda huko watawambia kila kitu kiko sawa watu endeeleni na kazi kwa sababu kuna mambo wanapata wenyewe huko.

Ni huzuni kubwa na ni aibu kuona kwamba watu wanakufa na wengine wanaangalia biashara kuliko maisha ya wananchi. Nasema, kwa maoni yangu nashukuru kwa hiyo Ripoti

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

lakini pia tupange kama Bunge tena ikiwezekana wiki ijayo kuweza kufunga hizo kampuni zote kwa sababu maisha ni muhimu kuliko jambo lengine lolote halafu tuweze kujua kwamba tumesimamisha sisi wenyewe maanake ndio ambao tumetunga sheria ya kusimamisha hayo machimbo huko.

Nataka niambie ile familia iliyopoteza huyo mtoto iwe pole na Mwenyezi Mungu aifariji. Niwatakieni tu kila la heri katika muhula huu ambao tunaenda kwa mapumziko marefu. Naomba turudi hapa salama tukiwa hatuna majeraha kwa sababu tulipoenda kule Bonde la Ufa, mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna majeraha ndani ya viwanja na nje ya viwanja lakini hata hivyo tulirudi salama. Tuonane Mwenyezi Mungu akipenda. Asanteni sana.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Mkumbi (Mariam).

Hon. (Ms.) Mariam: Asante, mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa hii tena. Hili swala la Jaribuni mimi nikiwa mmoja wa wale Wanakamati wa Utekelezaji ambaye pia niliambatana na hiyo Kamati na kuangalia ile hali halisi ya Jaribuni. Jaribuni kunatolewa raslimali nyingi sana ambayo inapeana pesa nyingi lakini ukiangalia maisha ya watu wa Jaribuni na zile pesa ambazo zinatoka Jaribuni havilingani, Bw. Spika. Ni mambo ya kusikitisha sana na ni mambo ya kuumiza moyo.

Kitu chengine ambacho nataka kuzungumza ni hii tabia ya kuwa Kamati inayohusika imepeana *recommendations* na haifuatwi na mtu. Hili ni jambo la kuudhi sana, yaani hii Kamati na hawa wanakamati kukaa na kuandika hizi *recommendations* na kupeana walikuwa hawana kazi ya kufanya. Hata wewe ambaye unaambiwa kuwa ufanye hivi na hivi hufanyi hata moja kwa sababu sisi kama Kamati ya Utekelezaji tuliangalia zile *recommendations* kama zilifanyika na hakuna *recommendation* yoyote ambayo ilifuatwa ambayo sasa hilo ni jambo ambalo wewe kama mwakilishi unajiuliza, *Executive* ina shida gani ama hawa Mawaziri wana shida gani?

Saa nyingine nataka kuungana na mheshimiwa Chengo ya kuwa nafikiri ikiwa hii Kamati haiwatoshi basi waletwe katika ile Kamati ya *General Oversight* hawa Mawaziri kwa sababu hatuwezi kuwa sisi tunakuja hapa kuweka *resolution* halafu wao hawafuatilii. Hili jambo lazima tuhakikishe limesimama kabisa ndio sisi kama Bunge wajue sisi tuko na kazi ya kufanya na kazi yetu ya kufanya ni hiyo na lazima sisi tukipitisha kitu hapa na ikiwa wao ndio wafuatilie ama watekeleze, lazima watekeleze.

Hii Ripoti ya Kamati ya Utekelezaji, naiunga mikono sana na kidogo nataka kukuuliza ikiwa sisi kama Kamati ya Utekelezaji imefika hapa na tumeweka maamuzi yale ambayo tumeyaweka na hao ambao wanastahili kutekeleza hawatekelezi tunaenda wapi kwengine? Kwa sababu haya ni mambo ambayo yanasikitisha na nafikiri nimuunge mkono huyu kama hizi sheria tukitunga hazifuatwi twende tukazitekeleze huko ambako kuna hayo mambo yanayoendelea ambayo hayafai. Sisi, tukitunga tunatunga na zinakuwa kwenye makaratasi na labda wanaona hawawezi kuzifuata tuende mpaka hapo.

Swala lengine ambalo linauma sana ni ile shule na ile kampuni. Mimi natoka pale Kambe Ribe na kidogo niko sehemu ambayo kuna *blast* ambazo zinafanywa na ile Simba *Cement*. Ukiangalia hao ni watu wazima ambao wanakaa pale, itakuja kuwa hawa watoto wa shule. Wale watoto wa shule na zile *blasts* na ni watu ambao kuna vitu ambavyo vinaweza fanyika na ile *blast* ifanywe kidogo lakini kwa sababu wanataka kuwa na mali nyingi kwa pamoja wakipiga wanapiga na kiwango ambacho hata hakiruhusiwi kisheria. Tulipoenda na Waziri ama tulipokaa na Waziri kabla hata hatujaenda tulimuita sisi hapa na tulipokaa naye tukawa tunajaribu kumuuliza haya maswala kwa sababu kuna kampuni imetajwa hapa pengine jina lake

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

nimelisahau, ilikuwa hawakupewa kibali walikuwa wameambiwa wasifanye ile kazi lakini utapata kazi inaendelea.

Yaani wameambiwa wasifanye lakini wanafanya na nasikia ni wachina. Sasa wachina kwa nini watatize wakenya ambao tuko ndani ya Jimbo letu na tuko ndani ya nchi yetu. Nafikiri kuna mambo ambayo pia Serikali yetu ya Kaunti lazima iangalie na watilie maanani kwa sababu maisha ya watu ni muhimu zaidi. Wewe ukiwa kiongozi na unaruhusu watu wanakufa bure utamuongoza nani? Lazima hili swala tulichukulie na nguvu zaidi sisi sasa kama watungaji sheria. Na nataka nikomee hapo nikiwa na huzuni sana kwa sababu maisha ya watu wa Jaribuni yako hali mbaya sana, Bw. Spika. Asante.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Mkumbi (Mariam) anauliza kama haikutimizwa atafanyaje? Bibilia inasema asiyefanya kazi asile, kama hutakula unafanyikaje? Unakufa, kwa hivyo kama hawakutimiza nyingine ni *impeachment* ndio imebakia kwa sababu *resolution* zote Kamati hata ikiweka mpaka ipitishwe katika Bunge ikipitishwa kwa Bunge huwa ni jukumu la Waziri mhusika atomize; kama hakutimiza ndio imewekwa hii Kamati iwe inaenda kufuatilia yale maamuzi ambayo tulifanya kama Bunge.

Kwa hivyo, ikiletwa Ripoti kama hii na ikipitishwa na haitatimizwa ni kumaanisha ameshindwa na kazi. Kwa hivyo, itakuwa hilo jino ni lingolewe ndivyo inakaa kisheria na iko vizuri imeandikwa kwa wino ambao ni mzito zaidi. Kwa hivyo, haina haja ya kuuliziwa labda kwa wale ambao hawakuwa wanafahamu kwamba lazima wafanye hivyo. Mambo mengi huwa yanaharibika kwa sababu nafikiri umemsikia mheshimiwa Chengo (Mumba) wa Tezo akisema kwamba kwa mara ya kwanza toka awe hapa ambayo saa hii ni mwaka wake wa saba ameona hii Kamati ikifanya kazi, Hii Kamati kama haifanyi kazi ndio itakuwa uamuzi wa Bunge hauwezi kutekelezwa. Lakini hii Kamati kazi yake ni kufuatilia zile Kamati zote na ule uamuzi ambao unaletwa hapa Bungeni kama utafanyiwa marekebisho ama ukiritimba halafu upitishwe unatakikana ufuatilizie. Je, kama iliambiwa ndani ya miezi mitatu na imefanya kazi, mmefanyiwa yale ambayo Bunge liliamua.

Kama uamuzi haukufanywa, wanaleta Ripoti kama vile wameleta leo na ikimaliza namna hiyo hakuna haja tena ya kupelekwa sehemu nyingine. Ile inayofuatilia sasa ni kumaanisha sikio la kufa halihitaji nini? Namalizia na hapo. Kwa hivyo, hakuna haja ya kuuliza swali kama hilo; swali tuko nalo sisi kwa sababu sisi ndio macho ya wale walituchagua tuje hapa, si ndio? Kwa hivyo, sisi ndio wa kuamua kama imeshindikana hawezi kufanya kazi, hii Kamati ina jukumu kubwa zaidi. Ndio inaweza fanya Kilifi iende mbele ama isiende mbele kwa sababu kazi yao ni kufuata nyuma yale ambayo mumeamua hapa. Kwa hivyo, si kusema *aye* tu muende nyumbani; ukisema *aye* pia inafuata nyuma. Mheshimiwa Ngome wa Mwawesa (Kalama).

Hon. Kalama: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for this opportunity. My submission is based seriously on the issue of unattended County Assembly resolutions. It has become a tendency of the Executive. Finally, there is a certain philosopher who said that justice delayed is justice denied. The Executive should take things seriously, otherwise this House will lose meaning. With those few remarks, I support the adoption. Thank you.

Hon. Brown: Asante, Bwana Spika, kwa muda huu ambao umenipatia. Nashukuru Mungu ni buheri wa afya siku ya leo. Mimi katika Ripoti hii ya Jaribuni ni Ripoti ambayo imenipatia mshangao mkubwa kwamba Kilifi yetu inaelekea wapi. Huwezi kuweka moja na hiyo hiyo moja ambayo umeiweka mwengine anaondoa, tutabaki na nini?

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hapa kuna kazi ambayo inafanyika. Nina kubaliana na maamuzi yaliyozungumzwa; kazi iliyobaki ni sisi tusimame kidete. Sasa mimi la kwangu nilikuwa naomba nizungumze ndani ya Bunge hili maswala matatu.

Swala la kwanza; ni lazima tusimame kidete tuondoe huu ubepari. Kuna ubepari ambao mara nyingi hausikii dawa na tukiwa hapa Bunge kama sisi ni wanasheria huu ubepari tuna uwezo wa kuamaliza, kama vile ulivyozungumza. Haiwezekani kwamba ndani ya Bunge kila kitu kiko dhahiri, watu wanaangamia, watu wanapata shida, watoto wanaangamia, afya inazorota lakini sisi tuko hapa tu tunaangalia mambo yanaendelea hivi hivi. Hilo haliwezekani! Na tukisema kwa kauli moja kwamba hii haiwezekani, tutaweza kutimiza maswala ya wanakilifi.

Mimi nahuzunika. Wiki nzima sijakuja Bunge na maswala ni hali kadhalika. Watu wanajenga kiholela holela pasipo na sheria. Mahali kwa ufuo wa maji mtu anajenga kampuni, wananchi mahali waliko maji yanatoroka yanafwata wananchi mahali ambapo siko, tunaelekea wapi? Ndio swali langu nilikuwa nimeanzia, sisi tunaelekea wapi? Majibu ya maswala haya tuko nayo sisi Wabunge ambao tulichaguliwa hapa Kilifi.

Jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba sisi kama wanasheria ambao tuko hapa ni lazima tuhakikishe kwamba utekelezaji ufanywe pasipo uzembe. Maofisaa ambao ni wazembe kwa kazi wanazembea, tuhakikishe kwamba tunawaondoa. Tukifanya moja tu kwa mfano wengine wote watakuwa wamelainika. Ni kweli, sisi tunahitaji kazi na yule mwenye kampuni akija, anaajiri watu na wanapata kazi.

Pili, tunapata pesa za Kaunti lakini tukiangalia wanaofaidika ni wachache. Je, sisi tuko hapa, la kufanya ni nini? Naomba tuhakikishe kwamba jinsi Bunge hili lilivyoamka na ninajua kabisa uwezo tuko nao; tuhakikishe kwamba tuna usimamizi wa kisawa sawa.

Mimi sina mengi yangu ni kuwatakieni siku kuu njema yenye heri na baraka na mwaka mpya wa fanaka mpaka mwakani tena tuonane kama tulivyo. Asanteni sana.

The Speaker (Hon. Mwambire): Dr. Ziro from Mwanamwinga, your friends normally notify me that you are an expert in minor operations.

Hon. Ziro: Asante sana, Bwana Spika, kwa hii nafasi. Kwanza kabisa, ningetaka nipongeze Kamati ya Utekelezaji ikiongozwa na mheshimiwa Changawa. Kulingana na ile Ripoti ambayo tulipewa na ile ambayo wametosomea ni kwamba wanafanya hii kazi bila uoga. Na mimi, ningetaka niwapongeze kwa hii shughuli; najua ni ngumu.

Pia kama Kiongozi wa walio Wachache alivyosema, nitataka niwaambie pole kwa ile kazi nyingi ambayo mnafanya na mapato ni kidogo ambayo yanaweza fanya mtende kazi hiyo yote. Mwenyekiti wa Bajeti ako hapa na bila shaka atachukulia hili jambo na uzito maanake hata mimi kuna Ripoti zetu za Afya ambazo pia tunazisubiri hapa Bungeni tujue mwelekeo wake uko namna gani. Wananchi wetu wanaumia na tuko na imani kwamba Kamati hii na hii kazi yao ndio itafanya tuone sura ya mabadiliko hapa Kilifi Kaunti.

Swala hili la jaribuni, sisi kama Kamati ya Afya tulifika Jaribuni. Kusema kweli ni jambo la kuhuzinisha na ni jambo la kutamausha na ni jambo ambalo linatuacha vinywa wazi. Kama wanakamati walifika kule, wakapeana mapendekezo yao na kufikia sasa hayajafanyiwa kazi. Mimi ninaunga Ripoti hii na ningetaka kuunga mkono Mwenyekiti wa Kamati hii kwamba ndani ya wiki mbili mabadiliko lazima yawe yameonekana pale Jaribuni.

Ni kweli kwamba watoto wanaumia kwa sababu zile kampuni zimejengwa karibu na shule na pia mbali na hayo kulingana na yale maswala ambayo tuliweza kupata Jaribuni, ni kwamba mbali na maswala ya shule wakaazi wa Jaribuni wanaumia.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mheshimiwa Jambo amegusia moja tu ya kwamba wazee wanafanya kazi ngumu ili kwamba wapate watoto lakini watoto wanaishia wakitoka kabla siku zao hazijafika. Hilo jambo ni la ukweli na tulilipata wananchi wakilizungumzia pale Jaribuni kwa huzuni kubwa sana.

Mimi nasimama kuunga mkono Ripoti hii na ndani ya wiki mbili, tuone mabadiliko na kama hakuna mabadiliko basi ile sheria ya Bunge ichukue mkondo wake. Asante sana, Bwana Spika.

The Speaker (Hon. Mwambire): Our new convert Emmanuel Baya, Member for Marafa.

Hon. Emmanuel: Thank you, so much hon. Speaker, for this opportunity. Thank you, hon. Members for the sincerity of your contributions. This is a matter of life and death and I stand here to defend life. With that, therefore, I join the hon. Member of Jaribuni to defend the lives that are under threat in Jaribuni.

We are elected Members, and we are here to defend and implement the wish and willingness of our people. It is very sad, that this House with all its integrity, with all the powers that we have been given and mandated by the people of our respective Wards and then we pass something, and it does not happen or it does not take place or it does not get implemented.

The honourable Chairperson of the Implementation Committee has indeed done a wonderful job of defending and trying to bring to the attention of this House that something is happening, and lives are in a state of threat.

If environmental issues are not well taken care of, they are like cancer and if we engage in the business of corruption with matters of life, I think we are not supposed to be here. We are not supposed to be here!

I come back to you, hon. Speaker. As we have said, if these matters have passed and are not being taken seriously, the main step this House must take is to bring on board the CECM in charge of this Department to be here. This should be the next step.

We will not be quiet to see this impunity happening while I am in this House. I will join my friends, Hon. Members, and the people of Jaribuni to make sure that this should not persist. I became emotional because I am a husband, I am a father of sons and daughters and I know and feel the same with the people of Jaribuni. It is not soothing that we should not take it merely.

If we mean the people of Jaribuni are trying hard to make sure that they achieve their biological rights to make sure that this world is full, nobody should come here and start undermining those powers of implementing that very noble action of bringing people to this world. It is very sad. All the environmental issues that are to be taken should be measured and make sure that the environment should be peaceful.

(Applause)

Those who are standing there in objection maybe in times of corruption deeds, this House is going to hunt them. I join the Hon. Member for Kakuyuni that if the CECM will not implement by next week, even if he shall not, the Whole House can go and implement. How dare a child who is a future leader not get the proper environment to achieve his dreams in terms of education and yet we are here? This cannot happen. If that continues, then Members need to resign. If this will not be implemented, then all Members should also resign and we are not resigning because we are going to take action.

The people of Kilifi will know that we are here, so let's take the correct steps so that this issue can be taken either peacefully or forcefully. I do not mind which way it may take but it

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

should be implemented. Thank you so much for this opportunity and I stand again to commend the job well done by this Committee and this is the way to go. We should not whatsoever jeopardize the efforts of this Committee on Implementation.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Morgan Kubo.

Hon. Kubo: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Nimesimama kuunga mkono Kamati hii kwa sababu najaribu kufikiria kitu kimoja. Kule kwetu Kambe-Ribe kuna kampuni moja ambayo pia iko na *quarry*. Vile inavyotuhangaisha hiyo kampuni sisi Wadi ya Kambe-Ribe na Kaloleni na ni wadi mbili, je kule Jaribuni vile kuna kampuni zaidi ya moja kunakuwa namna gani? Ningeomba...

The Speaker (Hon. Mwambire): Jaribuni iko na kampuni 25.

Hon. Kubo: Sisi tuko na moja peke yake Simba *Cement* na wako pale kutengeneza pesa lakini hawataki kujali maisha ya wananchi wa kawaida wa Kilifi. Hii kampuni wakitaka kuvunja mawe kuna baruti wanapiga. Kabla wapige hizo baruti, wanapiga king'ora ati wakaazi wa Kambe-Ribe wahame pale kwanza na wakae kando kwa muda wa dakika ishirini (20), wapige baruti halafu ndio warudi kuendeleza shughuli zao. Hii ni hali ambayo inasikitisha sana na kama haya mapendekezo yanaweza kufanyiwa kazi huko Jaribuni, nina hakika kwamba pia kule kwetu Kambe-Ribe hiyo kampuni moja ikisikia hivi, mambo mengi yatabadilika.

Nimesema niko na uchungu mwingi sana kwa sababu nimejaribu kusikiza haya mambo ni kama yale yanaoendelea kule kwetu pia. Naishukuru sana hii Kamati na naipongeza zaidi na naomba huyu Waziri afuatilizie haya mambo na kama hatafuutilizia kama vile mheshimiwa mwenzangu amesema, tutaungana sote twende kule kwa nguvu moja kama Bunge tuweze kuwaonyesha mfano bora zaidi.

Nikijua kwamba lile Bunge lilikuwa wakati mwengine, mambo mengi kama haya yaliletwa lakini hawakuyafuatilizia wakayamaliza waliyapuza na nisingependa hili Bunge liwe mfano kama ule. Hii Kampuni ya *Simba Cement* shida ilianza tangu miaka ya nyuma. Jambo hili lililetwa hapa pamoja na zile kampuni nyengine za *quarry* lakini mambo haya mpaka sasa, Mheshimiwa Spika, kusema ukweli bado yanaendelea, kuonyesha kwamba hayakufanyiwa kazi.

Ningeomba Bunge hili tushikane, tuonyeshe utofauti na Bunge lililopita na mambo yafanyike na tuweze kutetea mkaazi wa Kilifi. Kwa hayo mengi, naishukuru sana kwa nafasi hii na Mwenyezi Mungu awabariki. Asante.

The Speaker (Hon. Mwambire): Waheshimiwa, msije mkafanya watu wakafikiria kwamba mtaenda mkafunge kampuni. Uamuzi mtakaotoa hapa kuna ofisaa ambaye mmempatia mamlaka na sheria inamlinda kufanya juhudi kama hizo za kufunga kwa sababu mmeamua hivyo. Iwapo atashindwa, kwa mujibu wa sheria ni afunge virago aende nyumbani. Lakini sio nyinyi mkasukumane na kampuni na kuna mtu mmemtuma. Na mkienda kule ni awe yuko nyumbani ndio mnaenda. Kwa hivyo, ni mjue majukumu yenu na vile hali iko. Msisisitize sana kwa sababu hiyo ni kama wanaharakati lakini umekuja kuwakilisha.

Hapa unafanya kazi tofauti ya utunzi wa sheria, na uamuzi unaoweka hapa ni muhimu zaidi, ndio sababu unaambiwa kwamba uamuzi unaotoa wewe uko sawia na uamuzi ambao umetolewa na mahakama kuu. Kwa hivyo, kama uamuzi umeutoa hautatimizwa, uende ukashike mtu ufunge wewe, si hata mahakama ikisema afungwe, unafungwa? Askari atakuja, akuchukue maana mahakama imesema, ushikwe uwekwe ndani.

Kwa hivyo, ule uamuzi mnatoa ni kama haukutimizwa, yule afisaa ambaye anahusika anabeba jukumu. Hawezi itwa hapa kwa sababu hatuwezi kumuita na barua ya kusema tumekuja

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kukuulize kwa nini tusikufute kazi? Huwa ameshindwa na majukumu, kwa hivyo anafunga virago aende kwao.

Kwa hivyo, yanayokuja hapa inakuwa ni Hoja ya kutokuwa na imani naye ama Hoja ya kumng'oa mamlakani kwa sababu ameshindwa kutimiza. Ndio sheria inavyosema, lakini haisemi nyinyi mtoe uamuzi galafu mfuatilie. Kamati ya kufuatilia itoe uamuzi na nyinyi mchukue bakora na majembe kwenda kufunga. Sasa itakuwa hakuna haja hata ije hapa mngekuwa mmebaki kule nje mkatimiza hayo lakini, mmekuja hapa mkijua mnafanya jambo ambalo ni zito zaidi. Kwa hivyo, msiwe na hofu lakini mjue uamuzi mtakaotoa hapa kwa mara ya kwanza utakuwa ni mzito ziadi. Mlitoa uamuzi wa kwanza, ukadhihakiwa, huu mwengine hawawezi kudhihaki. Ni atimize, ama apishe mwengine achukue jukumu alitimize. Yeye awe yuko nyumbani. Mheshimiwa Elina Mapenzi.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Asante, Mheshimiwa Spika. Kwanza nishukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai; tuko wazima tunafunga Bunge salama isipokuwa mheshimiwa Zia ambaye hasikii vizuri lakini Mungu pia nawe atamshushia uponyaji na atainuka. Tumekuwa na safari za hapa na pale wengine tumeenda ulaya tumerudi salama, ni kumshukuru Mungu tu kwa rehema za safari.

(Laughter)

Mheshimiwa Spika, ninasimama kwa swala hili la Jaribuni ambalo tunalijadili kwa sasa. Kwanza, nataka kusema inahuzunisha kwamba hivi leo tunajadili swala hili kwa mara ya pili. Kamati ya Mazingira na Maji ilishughulikia swala hili nikiwa Naibu wa Mwenyekiti. Tulikuwa na ziara kule Jaribuni tukakalisha wananchi ambao tunawawakilisha wakatuelezea shida zao na tukakaa kama Kamati, Bunge likatumia fedha tukaenda andika Ripoti tukaja na mapendekezo ambayo baadaye hayakutekelezwa. Kwa mara ya pili tena, Bunge likatumia pesa kupeleka Kamati ya pili ya Utekelezaji kwa sababu ya utepetevu wa ofisaa ambaye tulimuweka pale kufuatilia maswala yanayopitishwa hapa yaweze kutekelezwa naye hafanyi hivyo.

Bunge limetoa fedha zake tena kwa mara ya pili kupeleka waheshimiwa Jaribuni kushughulikia swala hilo moja. Kwangu mimi naona ni madharau makubwa kwa hili Bunge na ni kama kazi yetu haitambuliki. Maanake kama tulichagua maofisaa ambao tunashirikiana sisi tukipitisha na ule upande mwengine kumelegea, basi mheshimiwa Changawa imefikia wakati utuletee ofisaa huyu kwa *Committee on General Oversight* tukirudi tu kutoka *recess*.

Tunataka aje atueleze ni nini kinamzuia na ni nini kinajiri kutekeleza yale ambayo Bunge limepitisha mahali hapa. Baada ya hapo tutajua ni hatua gani tutazifuata. Lengo letu ni mapendekezo ya Bunge yafuatilizwe maana tuko hapa kuwakilisha wale wengi ambao hawajaweza kufika mahali hapa. Itakuwa ni huzuni ikiwa wananchi wanaumia huko chini na sisi tuko hapa tunashughulika ila kuna mmoja anatumia nyuma katika jitihada zetu.

Nashukuru vile waheshimiwa wamekuja na muamko mpya; inakaa mheshimiwa Spika ile safari ya Dubai ilikuwa nzuri sana. Mwenyekiti wa Bajeti naona mambo yake si mabaya maanake ni mkali sana na anataka tuende kule haraka sana lakini tutafuata sheria vyenye inatuelekeza na hatimaye tutapata jibu la swala la Jaribuni. Asante.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Biryia Jonathan.

Hon. Rafiki: Asante Mheshimiwa Spika, *for the record*, mimi ni Mheshimiwa Rafiki. Nimekuja kuchelewa natumia kadi ya Mheshimiwa Biryia.

The Speaker (Hon. Mwambire): Ooh, Hon. Rafiki, proceed.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Rafiki: Asante, mheshimiwa Spika. Mimi ni Mwanakamati wa Kamati ya *Implementation*. Nilijaliwa siku moja kuenda kule Jaribuni na ile hali inaendelea kule ni dhambi. Kuna kiwanda nilienda kukiona na sikijui jina lakini mita 50 kutoka kwa hicho kiwanda kuna shule ya *primary school*. Nilipofika pale niliona watoto wanacheza lakini lile vumbi vile linavyokuja ni uangalie upande moja kwa sababu linakuja na nguvu nyingi. Niliuliza mwalimu mmoja kwa mfano huu upepo ukiwa mwingi mnafundisha vipi hawa watoto? Kumewekwa ka *fence* kadogo ka mabati ka *level* ya chini kidogo. Akanambia hapa mahali, mheshimiwa, pana shida hata ni Mungu atusaidie. Mtu akifika kiwango hicho basi huwa amepoteza imani kama anaweza kupata msada mahali popote.

Nilipofanya utafiti nikaona shida kubwa ni uzembe wa maofisaa wetu wa serikali yetu ya Kaunti. Zile kampuni zina leseni ya kibiashara na za NEMA (*National Environment Management Authority*). Kuna shida kule mahali kwa sababu wale watu wanaumizwa na maofisaa wachache sana. Mimi nimesimama nikisema tuna jukumu la kutetea watu wetu na najua matumaini makubwa ya wananchi ni hili Bunge. Mimi sitakaa hapa kuangalia maofisaa wachache wakidhulumu watu wetu; ni makosa sana.

Ninaunga mkono Ripoti hii na mwisho niwaombe the *Special MCAs* ambao wamejaliwa kuenda safari zaidi ya tano na wenzao wakiwa wamewawacha hapa, Mungu awasaidie waweze kuenda mpaka 2027 maana hicho kipindi chaishia hapo.

(Laughter)

Maana sielewi, mheshimiwa Spika. Nawatakia *Christmas* nzuri na mwaka mpya mwema wenye mafanikio. Mungu awajalie na afya njema tukutane tena hapa mwakani Mungu akipenda. Mimi niko nyumbani pale mnajua mtu akinialika napatikana. Asanteni.

The Speaker (Hon. Mwambire): Let the Mover respond please, Hon. Changawa.

Hon. Changawa: Thank you, Mr. Speaker. I want to thank all Members who have contributed to this Motion and even those who have not contributed. I am hoping they will contribute positively when you pose the Question. With those few remarks, I say thank you.

(Question put and agreed to)

BILL

First Reading

THE KILIFI COUNTY FINANCE BILL, 2023

(Order for First Reading read - Read the First Time and ordered to be referred to the relevant Departmental Committee)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

SUPPLEMENTARY BUDGET 2023/2024

The Speaker (Hon. Mwambire): Before we go to the last item, from the Communication I have issued today does not affect the Budget and Appropriations Committee Supplementary Budget of 2023/2024. We will have a brief meeting with the Chairperson and the Secretariat to decide on when we will be concluding the issues of the Supplementary Budget, possibly before Christmas.

Again, we will conclude together on the issue of the Report of the Committee on General Oversight. Tomorrow we will have a special meeting to deliberate on the issues of the Committee on General Oversight and later take a retreat on Friday to make a resolution on the same day we will be resolving the Supplementary Budget of 2022/2023.

To put it on record, the issues we will deliberate tomorrow will be in regard to the Department of Sports on the Supplementary Budget of 2022/2023 vote head 11109. So, Members, kindly avail yourselves tomorrow and be assured we will conclude this matter before we break for the Christmas season this year. We can proceed with the last item. Yes, Clerk?

I think I have already communicated the last item because there is no need for voting.

ADJOURNMENT

LONG RECESS-END OF THE SECOND SESSION

The Speaker (Hon. Mwambire): Pursuant to the provision of Standing Order 253 relating to the Calendar of the County Assembly and the resolution of the House, the Speaker notifies that upon the rise of the House at the appointed time today, regular sittings will resume on Monday, 12th February 2024 at 2:30 p.m.

Hon. Members, I wish you all the best as you prepare for this festive season. This House stands adjourned for the Second Session.

The House rose at 4:11 p.m.